

REVEALED NATIONAL EXAMINATIONS

SHULE YA SEKONDARI MTAWALIA

GREDI YA SABA

AWAMU 001

Jina:

Gredi:

Shule:

Nambari ya Usajili:

Mtihani Ya Gredi Ya Saba
2023

KISWAHILI LUGHA

Muda: saa 2 Dak. 10 na dakika kumi za kusoma

MAAGIZO KWA WATAHANIWA:

- Andika jina lako, nambari ya usajili, darasa na shule kwa nafasi zilizoachwa hapo juu.
- Usifungue karatasi hii hadi utakapoambiwa.
- Umepewa dakika kumi za kusoma maagizo. Usianze kuandika hadi uambiwe.
- Soma kila swali kwa makini.
- Jibu maswali YOTE.
- Andika majibu yako kwa wino mweusi au ya buluu katika nafasi ulizopewa kwenye karatasi hii.

KUTUMIWA KWA MKUFUNZI PEKEE

ALAMA

Alama Jumla	
Juu ya	
Asilimia	60

2
SEHEMUA

UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kisha uandike ufupisho wake.

Maji ni muhimu katika maisha ya binadamu, wanyama, ndege, samaki, wadudu na hata mimea. Ni kweli kuwa maji ni uhai. Maji hupatikana baharini, maziwani, mitoni na hata visiwani. Matumizi ya maji ni kama vile; kupukia, kuoshea, kunyunyizia mimea na kuwapa mifugo kunywa. Maeneo ya nchi ambayo hayana mito au mvua hayavutii watu wengi kuishi huko. Wenyeji wa sehemu hizo hukabiliwa na ukame.

Milima, misitu na maziwa huwa vianzo vya mito. Mlima Kenya huwa ni chanzo cha Mto Tana nayo Milima ya Cherengani na Mlima Elgon ni vianzo vya Mto Nzoia. Mito hii ni mionganini mwa mito muhimu katika nchi ya Kenya. Faida ya mito hii ni chungu nzima. Hutupatia maji ya matumizi nyumbani na viwandani, mito mingine hutumika kuzalisha nguvu za umeme na usafiri pia. Maji haya ya mito pia hunywewa na wanyama na vilevile huvutia watalii. Hivyo basi tunastahili kuyatunza maeneo mbalimbali ya maji.

Tusiharibu misitu yetu kwa kukata miti kiholela. Ikiwa tutakata mti mmoja, tupande miwili au zaidi. Ni jukumu la kila mmoja kuiyalinda mazingira yetu. Tusitupe takataka ovyo ovyo. Mvua inaponyesha huyabeba takataka zilizo tapakaa hadi katika mito. Wajenzi waviwanda pia wanatahadharishwa dhidi ya kuelekeza majitaka katika mito na maziwa.

1. Andika ufupisho wa kifungu hiki kuhusu umuhimu wa maji.

Zingatia yafuatayo:

- *Maneno yasizidi 60*
- *Iwe katika mpangilio kuendelea*
- *Iwe aya moja*

Tumia maneno yako mwenyewe bila kughairi maana ya kifungu. (alama 10)

7 SEHEMU YA D: FASIFI

Soma shairi hili kisha ujibu maswali

Wakati umeshafika, mimea kuitambua,
Mingi inayosifika, yatupasa kuijua,
Na matumizi twataka, tupate kuyaelewa,
Mimea tuisomeni, tuweze kuitambua.

Tuanze na mkahawa, jina jingine mbuni,
Huo huzaa kahawa, iuzwe ulimwenguni,
Ambayo yananunuliwa, tena kwa kubwa thamani,
Mimea tuisomeni, tuweze kuitambua.

Nao huo mpareto, nchini tunakuza,
Watuzalia pareto, maua ya miujiza,
Dawa yenyeye kubwa pato, Kwa mbu kuwafukuza,
Mimea tuisomeni, tuweze kuitambua.

Pia tusiusahau, mmea wa mzabibu,
Tuujuwe crgala, ndiye mama wa zabibu,
Zatumika kwa pilau, au kwenye matibabu,
Mimea tuisomeni, tuweze kuitambua.

Sote twapenda sukari, chaini inayotiwa,
Tulijueni vizuri, inayotokana na miwa,
Mikate hata mahamri, ni kawaida kutiwa,
Mimea tuisomeni, tuweze kuitambua
Someni bila dharau, mimea kuitambua,
Pia kuna mlimau, tusiache kuujua,
Mara watupa limau, kwa bei twalinunua,
Mimea tuisomeni, tuweze kuitambua.

Maswali

31. Shairi hili linahusu nini? (Alama 1)

32. Shairi hili lina beti ngapi? (Alama 1)

33. Andika vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa tatu. (Alama 2)

34. Ubeti wa pili una mizani ngapi? (Alama 2)

35. Andika kibwagizo cha shairi hili. (Alama 1)

36. Hili ni shairi la aina gani? (Alama 1)

37. Mimea ifuatayo huzaa nini? (Alama 2)

a) Mlimau _____

b) Mzabibu _____